**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI**


**SHULE YA SEKONDARI MBARALI,**

**S. L. P 156,**

**RUJEWA-MBARALI.**

**SIMU: 0755371276**


**TAREHE..............................**

**KUMB. NA. MBSS/JI/2020.............**

**JINA LA MWANAFUNZI.............................................................**

**S. L. P......................**

**RUJEWA – MBARALI**

**FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MBARALI KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2021 katika **shule ya sekondari Mbarali.** Shule ya sekondari **Mbarali** ipo kata ya Ubaruku wilaya ya Mbarali mkoa wa Mbeya. Mhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti na mzazi wako tarehe **11/01/2021 saa 1.30 asubuhi** bila kukosa. Mwanafunzi atapokelewa kuanzia tarehe **11/01/2021** hadi **18/01/2021** na baada ya hapo hatapokelewa. Shule ya sekondari Mbarali ni ya kutwa pia ni ya mchanganyiko yaani wasichana na wavulana.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1** ***Sare za Shule***

(a) Sare za shule hii ni kijani na kijivu kwa wavulana na wasichana. Wasichana sketi mbili zenye marinda na wavulana suruari mbili zenye rinda mbili. Aidha wasichana sketi ziwe ndefu na zikaribie kugusa kisigino vilevile zisibane. Wavulana suruari zisibane/zisiwe vimodo. Pia kwa wavulana mkanda mweusi ambao hauna pambo au chuma kikubwa.

(b) Mashati meupe ya mikono mifupi kwa wavulana na wasichana

(c) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba ambavyo havina visigino virefu (wavulana na wasichana)

(d) Soksi nyeupe kwa wavulana na wasichana (jozi mbili)

(e) Sare ya michezo ni fulana (T-shirt) na jozi moja ya raba kwa wavulana na wasichana

(f) Kwa wasichana wa kiislamu: Blauzi(nusu kanzu)-iwe ya mikono mirefu isiyofunika viganja vya mikono, iwe pana (isibane), iwe ndefu inayoshuka chini ya makalio (isiwe kama gauni) na isiwe nyepesi. Kitambaa cha kichwani (ushungi)-kiwe kipana, kiwe kirefu kisichofunika viganja vya mikono, kisifunike uso na kisiwe chepesi.

(g) Sweta ni la rangi ya damu ya mzee

**2.2** ***Vifaa vya Taaluma***

(a) Counter book kuanzia quire 2 na kuendelea ziwe 9

(b) Kalamu nyeusi au bluu zisipungue 3 na kalamu ya risasi (penseli) zisipungue 2

(c) Mkebe wa hisabati na vifaa vyake

**3.0** **<u>SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE</u>**

3.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi na kupewa nakala yako baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na kwa jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ni lazima.

(c) Kuwahi katika kila shughuli ya shule na nyingine utakazopewa.

(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.

(e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(f) Kuvaa sare ya shule muda wote unapotakiwa.

(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(h) Kutunza mali za uma.

**3.2** ***Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufutwa au kusimamishwa shule***

(a) Wizi

(b) Ubakaji

(c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, kokeini, milungi, kuberi n.k

(d) Kupigana au kupiga

(e) Kuharibu kwa makusudi mali ya uma

(f) Kudharau bendera ya taifa

(g) Kuwa mjamzito/ kupata mimba au kusababisha mimba

(h) Kuoa au kuolewa

(i) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

(j) Kukataa adhabu kwa makusudi

(k) Kuwa na simu ya mkononi

(l) Kutoa mimba

**4.0 Mambo muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi**

(a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii ikabidhiwe kwa mkuu wa shule punde utakaporipoti shuleni.

(b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

**5.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo au maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA MBARALI SEKONDARI**

**MARIA NGUVUMALI**

**MKUU WA SHULE**

**MEDICAL CERTIFICATE**

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING**

**MBARALI SECONDARY SCHOOL,**

**P. O. BOX 156,**

**RUJEWA – MBEYA**

**DATE...................................**

**TO MEDICAL OFFICER,**

**....................................................................**

**PART A**

**MR/MRS.........................................................................................**

Please examine the above named staff as to his or her physical and mental fitness.

The examination should include the following;

1. Haemoglobin.........................................................................................................

2. P. V bleeding.......................................................................................................

3. Sight.....................................................................................................................

4. Blood pressure....................................................................................................

5. Urine and sugar...................................................................................................

6. Stool for routine examination............................................................................

7. Pregnancy test........................................................................................................

8. Skin disease..............................................................................................................

9. Leprosy...................................................................................................................

10. Any deformity.........................................................................................................

11. Epilepsy..................................................................................................................

12. Pulmonary tuberculosis.........................................................................................

13. Neurosis...................................................................................................................

14. Veneral disease......................................................................................................

15. Other serious disease................................................................................................

**PART B**

(To be completed by a government medical officer)

1. I have examined the named staff and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for a full time schooling.

2. Other comments......................................................................

3. Date........................................Signature...............................................

4. Station....................................................................Official stamp.............................................